**MUHTASARI WA MKUTANO WA BARAZA LA MADIWANI KUJADILI TAARIFA ZA ROBO YA PILI KILICHOFANYIKA TAREHE 27/02/2024 KATIKA UKUMBI WA KANTINI BOMANI SENGEREMA.**

**A: WAHESHIMIWA MADIWANI WALIOHUDHURIA.**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mh. Makoye L. Sengelema | Diwani Kata ya Sima | M/M/kiti-H/W |
| 2. | Mh. Enock N. Sengelema | Diwani Kata ya Nyamazugo | Mjumbe |
| 3. | Mh. Fortunatus M. Nzwagi | Diwani Kata ya Kahumulo | " |
| 4. | Mh. Deus B. Masanyiwa | Diwani Kata ya Mwabaluhi | " |
| 5. | Mh. Deus M. Ndaki | Diwani Kata ya Igulumuki | " |
| 6. | Mh. Mathias M. Ng'henyenge | Diwani Kata ya Ibondo | " |
| 7. | Mh. Mbungai F. Majumba | Diwani Kata Mission | " |
| 8. | Mh. Charles M. Kagole | Diwani Kata ya Buyagu | " |
| 9. | Mh. George J. Kazungu | Diwani Kata ya Nyampande | " |
| 10. | Mh. Michael C. Masunzu | Diwani Kata ya Kagunga | " |
| 11. | Mh. Sadick J. Jimola | Diwani Kata ya Katunguru | " |
| 12. | Mh. Shokolo V. Joseph | Diwani Kata ya Kishinda | " |
| 13. | Mh. Simeo T. Busiya | Diwani Kata ya Nyamizeze | " |
| 14. | Mh. Godfrey M. Joseph | Diwani Kata ya Kasungamile | " |
| 15. | Mh. Sospeter S. Busumabu | Diwani Kata ya Tabaruka | " |
| 16. | Mh. Robert A. Madaha | Diwani Kata ya Chifunfu | " |
| 17. | Mh. Michael S. Mchele | Diwani Kata ya Nyatukala | " |
| 18. | Mh. Sanije F. Shibiliti | Diwani Kata ya Igalula | " |
| 19. | Mh. Dickson J. Samwel | Diwani Kata ya Busisi | " |
| 20. | Mh. Tryphone S. Male | Diwani Kata ya Kasenyi | " |
| 21. | Mh. Jumanne A. Masunga | Diwani Kata ya Ibisabageni | " |
| 22. | Mh. Igaga J. Sengasenga | Diwani Kata ya Bitoto | " |
| 23. | Mh. Kahogo A. Rajabu | Diwani Kata ya Nyampulukno | " |
| 24. | Mh. Donald N. Masindi | Diwani Kata ya Ngoma | " |
| 25. | Mh. Janeth M. Kasobi | Diwani Viti Maalum | " |
| 26. | Mh. Ashura T. Lutazi | Diwani Viti Maalum | " |
| 27. | Mh. Martha R. Shindika | Diwani Viti Maalum | " |
| 28. | Mh. Diana M. Buchard | Diwani Viti Maalum | " |
| 29. | Mh. Winfrida G. Mpanduji | Diwani Viti Maalum | " |
| 30. | Mh. Annastazia J. Kachawi | Diwani Viti Maalum | " |
| 31. | Mh. Modesta L. Bulugu | Diwani Viti Maalum | " |
| 32. | Mh. Marry L. Pastory | Diwani Viti Maalum | " |
| 33. | Mh. Betty Dackman | Diwani Viti Maalum | |
| 34. | Ndg. Binuru Shekidele | Mkurugenzi Mtendaji (W) | **Katibu** |

**B: WAHESHIMIWA WASIOHUDHURIA KWA TAARIFA**

| | | |
|---|---|---|
| 1. Yanga E. Makaga | Diwani Kata ya Nyamatongo | M/Kiti H/W |

**C: WATAALAM WALIOHUDHURIA**

| | | |
|---|---|---|
| 1. Ndg. Christina D. Bunini | Mkuu wa Divisheni ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimaliwatu | **Mjumbe** |
| 2. Ndg. Wilibard Bandola | Mkuu wa Divisheni ya Mipango na Uratibu | " |
| 3. Ndg. Michael Mapela | Mkuu wa Kitengo cha Usimamizi wa Manunuzi | " |
| 4. Ndg. Deocles Mushema | Kaimu Mkuu wa Kitengo ya Fedha na Uhasibu | " |
| 5. Ndg. Yusta A. Mwambembe | Mkuu wa Divisheni ya Maendeleo ya Jamii | " |
| 6. Ndg. Genoveva G. Chuchuba | Mkuu wa Divisheni ya Elimu Sekondari | " |
| 7. CPA. Silanda Mwidikila | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani | " |
| 8. Adv.Samara H. Matiku | Mkuu Kitengo cha Huduma za Sheria | " |
| 9. Ndg. Richard Bagolele | Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano serikalini | " |
| 10. Ndg. Benadetha S. Fransisco | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Maliasili na Uhifadhi wa Mazingira | " |
| 11. Ndg. Mallisa M. Ndugha | Mratibu wa TASAF (W) | " |
| 12. Ndg. Mwita M. Waryuba | Mkuu wa Divisheni ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi | " |
| 13. Ndg. Elias J. Mwita | Kaimu Mkuu Divisheni ya Miundombinu, Maendeleo ya Mijini na Vijijini | " |
| 14. Ndg. Edgar Heri | Kaimu Mkuu wa Kitengo ya TEHAMA na Takwimu | " |
| 15. Ndg.Tandi Laizer | Kaimu Mkuu Kitengo cha Taka ngumu na Usafishaji wa mazingira | " |
| 16. Ndg. Sylverster P. Mapunda | Kaimu Mkuu Divisheni ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji | " |
| 17. Ndg. Fortunatus M. Masaga | Kaimu Mkuu Kitengo cha Michezo, Utamaduni na Sanaa | " |
| 18. Dr. Fredrick Mugarula | Kaimu Mkuu Divisheni ya Huduma za Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe | " |
| 19. Ndg. Donati M Bunonosi | Mkuu Divisheni ya Elimu Awali na Msingi | |
| 20. Ndg. Fadhili W. Abel | Afisa Tarafa Sengerema | " |
| 21. Ndg. Simon M. William | Kaimu Mkuu Divisheni ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya na Makazi | " |
| 22. Ndg. Renatus Rukangakara | Afisa Mapato (W). | " |
| 23. Ndg. Hassan J. Hassan | Kaimu Afisa Usafirishaji (W) | " |

**D: WATAALAM WASIOHUDHURIA KWA TAARIFA**

| | |
|---|---|
| 1.Ndg. Happiness J. Segere | Afisa Tarafa Nyanchenche |
| 2.Ndg. Kaswahili Batalangile | Afisa Tarafa Katunguru |

**E: WAGENI WAALIKWA**

| | |
|---|---|
| 1. Mhe. Senyi Nganga | Mkuu wa wilaya ya Sengerema |
| 2. Mhe. Mark Agustine | M/kiti CCM (W) |
| 3. Mhe. Tasabam H. Mwaga | Mbunge Jimbo la Sengerema |

4. Ndg.Cuthbert B. Midala — Katibu Tawala (W).
5. Mhe: Rosemary J. Mwakilasu — K.n.y Katibu CCM (W)
6. A/ISP Juma Ngwembe — DFO
7. Ndg. Haji Mohamed — OCD
8. Ndg. Alfred V. Bogohe — DSO
9. Ndg. Yohane D. Maganga — DIO
10. Ndg. Prosper Temba — DPO
11. Ndg. Julius Mukulu — Ag. PSO
12. Sakila M. Budigila — M/Jeshi la Akiba
13. Ndg. Benedict Mrema — Ag. Meneja TANESCO (W)
14. Ndg. Sosthenes S. Tangalo — Ag. DCSQAO
15. Eng. Elisha P. Sembo — Ag. RUWASA
16. Eng. Prosper J. Francis — DM. TARURA
17. Ndg. Diomisius E. Rwezaula — REA

**F: WAGENI WAALIKWA WASIOHUDHURIA KWA TAARIFA.**

1. Ndg. Mussa Z. Malimi — Kaimu Meneja SEUWASA

**G: WAANDISHI WA HABARI**

1. Ndg. Idd Mumba — Global TV
2. Ndg. Deborah Maisa — Gazeti Nipashe
3. Ndg. Tunu Herman — TBC
4. Ndg. Anna Ruhasha — RFA
5. Ndg. Jama Jafari — Star TV
6. Ndg. Said. Mahera — Radio Sengerema

**G: WAANDISHI WA VIKAO**

1. Ndg. Anociatha B. Missingo
2. Ndg. Mbeba D. Masatu
3. Ndg. Emmanuel M. Masemele

**Muht.Na. 14/02/2024 - Kufungua Mkutano**

**Katibu:** Aliwakaribisha Wajumbe na waalikwa wote katika Mkutano, aliwaeleza kuwa ni Mkutano wa kisheria kwa ajili ya kujadili taarifa za robo ya Pili Oktoba hadi Disemba, 2023/2024. Kisha alimkaribisha Mwenyekiti ili afungue Mkutano.

**Mwenyekiti:** Alianza kwa kusoma Dua/Sala ya Halmashauri, kisha aliwasihi wajumbe kujikita katika kujadili agenda zote zilizowasilishwa, kutoa ushauri, maoni na mapendekezo yaliyo chanya ili kuleta tija kwa manufaa ya Wananchi wa Sengerema. Kisha alifungua Mkutano mnamo saa 06:03 Mchana.

**Muht.Na.15/02/2024 – Kuthibitisha Agenda za Mkutano**

Katibu aliwasilisha agenda ya kuthibitisha agenda za mkutano; Mwenyekiti aliwahoji wajumbe kama wanathibitisha agenda, hata hivyo waliongeza agenda moja kwa siku ya kwanza iliyohusu kutoa vyeti vya pongezi kwa Walimu na Shule (Sekondari na Msingi) zilizofanya vizuri katika matokeo ya Mitihani ya Taifa kwa Mwaka 2023. Wajumbe waliridhia kuthibitisha agenda zifuatazo:

**Mhe Mbunge wa Jimbo la Sengerema;** Alieleza kuwa matokeo mazuri ni juhudi zilizofanywa kuanzia kwa Mkurugenzi Mtendaji (W), Waheshimiwa Madiwani, Wataalam na Waalimu kwa usimamizi na ufundishaji mzuri. Aidha aliongeza kuwa matokeo ya shule za msingi siyo ya kuridhisha hivyo jitihada zaidi zinahitajika ili kufanya vizuri zaidi ikiwemo:-

i. Semina kwa Waalimu, ili kupata mbinu mpya ya ufundishaji kwa sababu mitaala imebadilika.
ii. Miundombinu haitoshi, hivyo zifanyike jitihada za makusudi za kuongeza miundombinu ili wanafunzi wapate mazingira mazuri ya kujisomea.
iii. Wakaguzi wa Shule wapite kwenye shule zote kuangalia mapungufu yaliyopo na zile ambazo zimekamilika zisajiliwe ili wanafunzi wapate fursa ya kutumia shule hizo.

**Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi (W):** Alieleza kuwa mafanikio hayo ni matokeo ya kazi inayofofanywa na Chama Tawala (Chama cha Mapinduzi) kwa kuleta fedha nyingi za Miradi ya Maendeleo, alisisitiza zaidi usimamiaji wa Fedha zinazoletwa zitumike kwa malengo ya Serikali yaliyokusudiwa. Vile vile aliwataka Waheshimiwa Madiwani pamoja na Wataalam kuendelea kuwahamasisha wazazi kuchangia chakula mashuleni. Wanafunzi wenye umri mdogo ili waelewe na kufuatilia wanachofundishwa mashuleni ni lazima wapate chakula.

**Katibu wa UWT Kwa niaba ya Katibu wa chama cha Mapinduzi:** alianza kwa kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhehimiwa Dr. Samia Suluhu Hassan kwa kujenga miundombinu mingi katika sekta ya Elimu na Sekta zote kwa ujumla wake. Aidha alishauri masuala kadhaa ya kufanyia kazi ili kuboresha zaidi kama ifuatavyo :-

a. Shule ambazo zina upungufu wa madawati, ambazo baadhi ya wanafunzi Wanakaa chini ufumbuzi wa changamoto hiyo ufanyike ili kuwawezesha watoto kukaa kwa kwenye madawati wakati wanafundishwa.
b. Watoto walio na umri wa kuanza shule/ kuendelea na shule mamlaka husika zihakikishe watoto wanahudhuria shuleni, alikemea tabia ya baadhi ya watoto wanauza ndizi na karanga muda wa masomo.

**Muht.Na.17/02/2024 - Maswali ya Papo kwa Papo.**
**Katibu** aliwasilisha agenda ya maswali ya papo kwa papo, Mwenyekiti alieleza kuwa hakukuwa na maswali ya papo kwa papo siku hiyo yaliyowasilishwa kwenye Ofisi ya Mwenyekiti.

**Muht.Na.18/02/2024 - Kusoma na Kuthibitisha Muhtasari wa Baraza robo ya kwanza wa tarehe 17/11/2023.**
**Katibu:** Aliwasilisha Muhtasari wa Mkutano wa Baraza wa tarehe 17/11/2023. Mwenyekiti aliwaongoza wajumbe kusoma na kupitia muhtasari wa Mkutano wa Baraza ukurasa kwa ukurasa. Wajumbe waliridhia muhtasari huo usainiwe na utunzwe kwa ajili ya kumbukumbu ya baadae.

**Muht.Na.19/02/2024 - Yatokanayo na Mkutano wa Baraza wa tarehe 17.11.2023.**
**Katibu:** Aliwasilisha utekelezaji wa Yatokanayo na Mkutano wa Baraza wa tarehe 17.11.2023. Mwenyekiti aliwaongoza wajumbe kujadili utekelezaji wa

yatokanayo/maazimio hayo. Wajumbe waliridhia utekelezaji wa maazimio hayo hata hivyo walishauri kuwa kasi ya utengenezaji wa Majoho uongezeke ili yakamilike na yaanze kutumika. Aidha walisisitiza ushirikiano kati ya Halmashauri na Taasisi za Serikali ili kufikia dhima ya maendeleo kwa Wananchi wa Wilaya ya Sengerema.

**Muht.Na.20/02/2024 - Baraza kupokea Taarifa za Maendeleo ya Kata.**
**Katibu:** Aliwasilisha agenda ya Baraza kupokea Taarifa za Maendeleo ya Kata. Mwenyekiti aliwaongoza wajumbe kupitia taarifa za maendeleo ya kata. Kisha wajumbe walishauri kuwa changamoto zote zilizopo katika kata ziorodheshwe na Mkurugenzi Mtendaji hatatue changamoto hizo, waliongeza kuwa katika Mkutano wa Baraza wa kujadili taarifa za robo ya tatu 2023/2024 kila Mhe, Diwani atawasilisha taarifa kutoka kwenye Kata yake. Kisha waliridhia taarifa hiyo.

**Muht.Na.21/02/2024 - Kuahirisha Mkutano.**
**Katibu:** alimkaribisha mwenyekiti kwa ajili ya kuahirisha mkutano, Mwenyekiti aliahirisha mkutano mnamo saa 7:14 mchana. Hata hivyo mwenyekiti aliwahoji wajumbe kama wanaridhia kuendelea kujadili agenda za siku ya pili.
Wajumbe waliridhia kuendelea na mkutano ili kujadili agenda za siku ya pili.

**Muht.Na.22/02/2024 - Kupokea Taarifa ya Utendaji Kazi wa Kamati za Kudumu za Halmashauri kwa kipindi cha robo ya pili Oktoba hadi Disemba 2023/2024**

**Muht.Na.23/02/2024 (I) - Kamati ya Kudhibiti UKIMWI.**
**Mwenyekiti wa Kamati ya Kudhibiti Ukimwi aliwasilisha taarifa ya Kamati ya Kudhibiti UKIMWI:** Alieleza kuwa Kamati ya kudhibiti Ukimwi imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria. Katika kutekeleza majukumu yake Kamati ilifanya kikao kimoja cha kisheria na katika kikao hicho Kamati ya ilipokea, ikajadili na kuridhia taarifa kutoka vitengo na wadau mbalimbali kama ifuatavyo: -

1. CHACC, DACC na Ustawi wa Jamii
2. KONGA
3. BAKWATA
4. VIJANA

Kamati ilishauri ushirikiano uendelee kuanzia ngazi zote za katika jamiii (Waheshimiwa Madiwani, Watendaji wa Kata, Wenyeviti wa Vijiji na Vitongoji pamoja na Wadau) ili kupunguza na kutokomeza maambukizi mapya ya VVU na Ukimwi. Kamati ilishauri Waheshimiwa Madiwani wawe mstari wa mbele kuhamasisha Kamati za Ukimwi ngazi ya Kata/Vijiji hadi Vitongoji ili kufanya vikao na taarifa za vikao hivyo ziwasilishwe ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji. Wajumbe walipokea taarifa hiyo wakaijadili, Kisha waliridhia taarifa hiyo.

**Muht.Na.23/02/2023 (II) - Kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira.**
**Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira:** aliwasilisha taarifa ya Kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira: Alieleza kuwa Wajumbe wa Kamati walitembelea Miradi Ifuatayo-
Mpango Miji eneo la Sotta – Ngoma: viwanja 744,Marekebisho ya Mpango Miji ya Nyabila – Ngomba: viwanja 349,Mchoro wa Mipango Miji wa Ngoma: viwanja 461,Maerkebisho ya Mchoro wa Mipango Miji wa Ngoma A: viwanja 31,Mchoro wa Mipango Miji wa Ngoma: viwanja 461,Mchoro wa Mipango Miji wa Sotta – Ngoma: viwanja 645,Mchoro wa Mipango Miji wa Sotta – Ngoma: viwanja 645.Mchoro wa

Mipango Miji wa Ibisabageni: Eneo hilo lipo Kitongoji cha Ibisabageni Kata ya Ibisabageni mchoro huo umendaliwa kutokana na baadhi ya Waathirika katika Mgodi wa Sotta Gold Mining kuhamishwa katika maeneo yao. Eneo hilo limezalisha jumla ya viwanja 441 vyenye matumizi mbalimbali

Vile vile Kamati ilipokea, ikajadili na kuridhia taarifa za utendaji kazi kutoka Divisheni na Vitengo mbalimbali za Halmashauri. Divisheni na Vitengo hivyo ni kutoka:

1. Kitengo ya Maliasili na Uhifadhi wa Mazingira
2. Kitengo ya Taka ngumu na Usafishaji wa Mazingira
3. Divisheni ya Miundombinu, Maendeleo ya Mijini na VIjijini
4. Divisheni ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi
5. Divisheni ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji
6. TASAF

Wajumbe walipokea taarifa hiyo, wakaijadili waliohoji ni lini maeneo ya mjini kati yatakuwa safi. Pia walishauri kuwa ifikie wakati ambapo uchafu mjini kati katika Halmashauri ya Sengerema ibaki historia hivyo kuwe na mkakati maalum wa kuufanya mji kuwa safi. Kisha wajumbe waliridhia taarifa hiyo. Wajumbe wa Kamati walifafanua kuwa hatua mbalimbali zinaendelea kuchukuliwa kuhakikisha maeneo yanakuwa safi ikiwemo kuhakikisha uchafu unazolewa kwa wakati.

***Azimio 1.***
***Iliazimiwa kuwa Mkurugenzi Mtendaji ahakikishe maeneo ya mjini Kati katika Wilaya ya Sengerema yawe safi.***

**Muht.Na.23/02/2023 (III) - Kamati ya Elimu, Afya na Maji.**
**Mwenyekiti wa Kamati ya Kamati ya Elimu, Afya na Maji:** Aliwasilisha taarifa ya Kamati ya Elimu, Afya na Maji alieleza kuwa ilifanya ziara moja ambapo ilitembelea:

**1. Shule ya Msingi Kijiweni iliyopo Kata ya Chifunfu.**
Lengo la ziara hiyo ilikuwa maendeleo ya shule hiyo ambayo kwa sasa ina wanafunzi takribani 1689 na Walimu 15. kamati ilibaini changamoto zifuatavyo, Ukosefu wa Umeme, hakuna maji ya bomba hususani kwa matumizi ya vyoo, Upungufu wa Madawati 280 na upungufu wa Waalimu 23.

**2. Kituo cha Afya Ngoma Mtimba Kata ya Chifunfu.**

a. Jengo la Wazazi na Upasuaji: Kamati ilibaini kuwa kituo hakijakamilika fedha iliyotolewa haikutosha, kuna upungufu wa Tzs 150,000,000.00 ili kukamilisha ujenzi wa kituo hicho. Kamati ilishauri kuwa yaandikwe maombi maalum ili fedha za ukamilishaji zitoke serikali kuu. Halmashauri itaendelea kuchangia ujenzi huo kupitia mapato ya ndani kadri fedha zitakavyopatikana.
b. Jengo la kufulia: Kamati ilibaini kuwa Jengo haijakamilika, Kamati ilishauri kuwa Mkurugenzi Mtendaji (W) afanye tathimini ya gharama ya kazi iliyobaki na BOQ iandaliwe ili kuweza kujua gharama kamili za ukamilishaji wa jengo hilo.

3. Shule ya Sekondari Chifunfu: Kamati ilipongeza shule kwa matokezo mazuri ya kidato cha nne mwaka 2023. Aidha Kamati ilipokea taarifa ifuatayo:-shule ina mapungufu ya madarasa 4, vyumba 3 vimekamilika bado kuweka madirisha na milango. Vile vile Kamati ilipokea taarifa za utendaji kazi kutoka Divisheni na vitengo mbalimbali za Halmashauri. Taarifa zilizopokelewa na kujadiliwa ni kutoka katika

i) Divisheni ya Elimu Sekondari
ii) Divisheni ya Elimu ya Awali na Msingi
iii) Divisheni ya Huduma za Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe
iv) Divisheni ya Maendeleo ya Jamii
v) Kitengo ya Michezo, Utamaduni na Sanaa

Wajumbe walipokea taarifa hizo, wakajadili, Wajumbe waliipongeza Kamati kwa matokeo mazuri ya kidato cha nne, Wajumbe walihoji yafuatayo:-

1. Upungufu wa shule za Msingi na Sekondari katika maeneo mbalimbali hali inayopelekea wanafunzi kutembea umbali mrefu, pamoja na upungufu wa Madawati ni lini changamoto hizo zitatatuliwa.
2. Ukosefu wa nyumba za walimu katika shule ya Mkomba kata ya Busisi na nyumba iliyopo ni mbovu inahitaji ukarabati.
3. Wanafunzi wa kike ni lini wataanza kupatiwa taulo za kike ili wasikose vipindi vya masomo.
4. Ujenzi wa chuo cha Ufundi Tabaruka.

Kamati walifafanua kuwa upungufu wa shule na Madawati, changamoto hiyo inafanyiwa kazi, mwaka wa fedha 2024/2025 kuna maombi ya ujenzi wa shule katika maeneo mbalimbali. Kwa upande wa Madawati Mhe; Mbunge wa Jimbo la Sengerema alieleza kuwa hatua mbalimbali zimechukuwa ikiwemo kuwaandikia barua Wakala wa Misitu Tanzani (TFS) ili watoe mbao kwa ajili ya utengenezaji wa madawati. Aidha Mkurugenzi Mtendaji aliongeza kuwa tayari Mgodi umeridhia kutoa madawati kutoka kwenye CSR ili kupunguza upungufu huo.

Suala la ukosefu wa nyumba za walimu Kamati ilieleza kuwa siyo la Kata ya Busisi peke yake ni la Halmashauri nzima, hivyo kuna baadhi ya shule ambazo zimeingizwa kwenye mpango na Bajeti ya 2024/2025 kwa ajili ya kujengewa Nyumba za Waalimu. Vile vile Mhe; Mbunge wa Jimbo la Sengerema alishauri kuwa wazazi washirikishwe ili wachangie ukarabati wa shule ya Msingi Mkomba iliyopo Kata ya Busisi. Mkurugenzi Mtendaji alieleza kuwa kuhusu taulo za kike, Halmashauri inafanyikia kazi mchakato ukikamilika taulo hizo zitaanza kugawiwa mashuleni. Kuhusu ujenzi wa chuo cha Ufundi Tabaruka Mhe; Mbunge wa Jimbo la Sengerema, alieleza kuwa bajeti iliyokuwa imetengwa kwa ajili ya ujenzi wa chuo hicho imependekezwa ipelekwe katika Halmashauri ya Buchosa kwa sababu hakuna chuo cha ufundi chochote hata hivyo alieleza kuwa chuo cha Ufundi kilichopo Sengerema kitaboreshwa zaidi.

**Muht.Na.23/02/2024 (IV) - Kamati ya Maadili.**

**Mwenyekiti Kamati ya Maadili aliwasilisha taarifa ya Kamati ya Maadili robo ya kwanza Pili (Oktoba hadi Disemba), 2023:** Alieleza kuwa Kamati ya Maadili Katika kutekeleza majukumu yake kwa kipindi cha robo ya pili Oktoba hadi Disemba, 2023/2024: Kamati imefanya kikao kimoja cha kisheria, ambapo Wajumbe walijadili Kanuni za kudumu za Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema za mwaka 2014, Kanuni zilizojadiliwa:

i. Kanuni namba 5 “Mkutano wa Bajeti”
ii. Kanuni namba 11 “Kumbukumbu ya Mahudhurio”
iii. Kanuni namba 22 “Maswali”
iv. Kanuni namba 23 “Maswali ya papo kwa papo”
v. Kanuni namba 25 “Taarifa za kutoka kwenye Kata”

Aidha kamati ilishauri kuwa katika mikutano ya Baraza (Baraza Chama, WDC na Baraza Full) taarifa za Kata zitakuwa zinawasilishwa na Mhe: Diwani wa Kata Husika. Wajumbe walipokea taarifa hiyo, wakaijadili kisha waliridhia taarifa hiyo.

**Muht.Na.23/02/2024 (V) - Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango.**
**Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango Aliwasilisha taarifa ya utendajikazi kamati ya fedha, uongozi na mipango robo ya pili Oktoba hadi Disemba 2023/2024** Alieleza kuwa Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango katika robo ya pili kuanzia Oktoba hadi Disemba, 2023 ilifanya ziara ya kutembelea Miradi. Vile vile Kamati ilipokea ikajadili na kuridhia taarifa za utendaji kazi kutoka Divisheni na Vitengo mbalimbali za Halmashauri.
**Taarifa za utendaji kazi kutoka Divisheni na Vitengo mbalimbali za Halmashauri**

**zilipokelewa zikajadiliwa na kuridhiwa ni:-**

1. Taarifa ya Miradi ya Maendeleo
2. Taarifa ya Kitengo ya Usimamizi wa Manunuzi
3. Taarifa ya Divisheni Utawala na Usimamizi wa Rasilimaliwatu
4. Taarifa ya Kitengo ya Ukaguzi wa Ndani
5. Taarifa ya Kitengo ya Huduma za Sheria
6. Taarifa ya Kitengo ya Tehama na Takwimu
7. Taarifa ya Kitengo ya Mawasiliano Serikalini

**Mradi wa Ujenzi Jengo la Utawala:** Lengo la ziara hiyo ilikuwa ni kuangalia na hali ya ujenzi wa Jengo la Utawala unaondelea, hatua iliyopo ni ni kufunga formwork ya kumwaga ribim, ujenzi umefikia 65%
Wajumbe wa kamati waliridhika na hatua ya ujenzi huo unavyoendelea, walisisitiza kuwa Mkandarasi aongeze kasi ya ujenzi ili kukamilisha ujenzi huo kwa wakati.
**Shule ya Msingi Nyamtelela iliyopo Kata ya Katunguru:** Kamati ilibaini upungufu wa matundu ya vyoo, yaliyopo ni mawili ambayo wanatumia Waalimu na Wanafunzi. Kutatua changamoto hiyo Serikali ya Kijiji kwa kushirikiana na Wananchi wamejanga matundu 11 ambayo yapo ngazi ya Lenta. Kamati iliahidi kutatua changamoto hiyo ya ukosefu wa vyoo.
**Shule ya Msingi Nyamililo iliyopo kata ya Kasungamile:** Kamati ilibaini kuwa vyoo vimetitia lakini kuna jitihada za Wanachi za ujenzi wa matundu 4 ya vyoo ambayo yapo hatua ya Lenta. Aidha kamati ilishauri kuwa itengwe fedha kutoka mapato ya ndani kwa ajili ya ukamilishaji wa matundu hayo.
**Shule ya Msingi Ibisabageni iliyopo Kata ya Ibisabageni.** Kamati ilibaini upungufu wa matundu ya vyoo, yanayofanya kazi ni 2 ambayo yanatumika na walimu pamoja na Wanafunzi. Kamati iliahidi kutatua changamoto hiyo kupitia vikao vyake vya Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango.
**Stendi ya Bukala iliyopo Kata ya Ibisabageni.** Kamati ilibaini mashimo katika stendi ya Bukala, aidha ilimuagiza Mkurugenzi Mtendaji kufanya tathimini ya matengezo ya Stendi hiyo.
**Shule ya Msingi Shikizi Bugeshi iliyopo Kata ya Nyampande:** Lengo la Ziara ilikuwa kuona hali halisi ya ujenzi wa Shule hiyo ulipofikia, gharama za ujenzi mpaka ni Tzs 34,252,000.00. Kuna vyumba 4 vya madarasa na Ofisi 1 ya mwalimu

vimekamika hadi hatua ya Lenta. Vyumba 4 vya madarasa havijafungwa lenta. Uongozi wa Kitongoji cha Bugeshi waliomba Halmashauri wasaidie kumalizia ujenzi wa maboma hayo, aidha Wananchi wapo tayari kuendelea kuchangia michango waliojiweke ili kukamisha ujenzi wa shule hiyo. Kamati ilichukua maombi ya wananchi hao na kuahidi kufanyia kazi.

**Shule ya Msingi Nyashimba iliyopo Kata ya Igalula:** Kamati ilijiridhisha kuwa vyumba 2 vya madarasa viliezuliwa na upepo tarehe 15/10/2023 Kamati ilichukua changamoto hiyo ili ikafanyiwe kazi katika Kikao cha Kamati ya Fedha,Uongozi na Mipango.

Mbali na kutembelea miradi, Kamati ilipokea na kujadili taarifa ya Majina ya Wajumbe, wa Bodi ya Afya Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema, Taarifa ya Magari na Mtambo wa Halmashuri na taarifa ya mapato na matumizi robo ya pili 2023/2024.

**TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI ROBO YA PILI 2023/2024**

**Mapato:** Halmashauri ya wilaya ya Sengerema ilikadiria kukusanya/kupokea jumla ya Tzs 53,232,958,555.00 kutoka katika vyanzo mbalimbali. Aidha fedha zilizovuka mwaka (bakaa ya mwaka wa fedha 2022/2023) Mapato ya ndani ni Tzs 49,444,466.51, Akaunti ya Miradi ya Maendeleo Tzs 534,804,772.58 nakufanya jumla kuu kuwa Tzs 53,883,352,494.09. Kipindi cha mwezi Disemba, 2023 Halmashauri ilikusanya na kupokea jumla ya Tzs 8,603, 352,797.80 ikiwa ni sawa na 193.78% na mapato ya Julai –Disemba 2023 ni Tzs 21,560, 987,436.58 ikiwa ni sawa na 56.97%. Mapato ukilinganisha na makisio ya mwaka hadi kufikia mwezi Disemba 31. 2023 Halmashauri imekusanya na kupokea Jumla ya Tzs 21,560, 987,436.58 Ikiwa ni sawa na 40.50% ya lengo la mwaka la kukusanya na kupokea Tzs 53,232,918,555.00 ya bajeti iliyoidhinishwa. Kwa upande wa Makusanyanyo ya ndani ya Halmashauri jumla ya Tzs 1,206,668,160.06 zimekusanywa ikiwa ni sawa na 40.06% ya lengo la mwaka la kukusanya jumla ya Tzs 3,012,492,555.00 kutoka katika vyanzo vyake mbalimbali vya ndani halisi na fungiwa. Mapato ya ndani halisi ni Tzs 910,676,922.00 sawa na 35.94%ya lengo la mwaka la Tzs 2,533,742.555.00.

**Matumizi:** hadi kufikia mwezi Disemba 2023, Halmashauri imetumia jumla ya Tzs 26,775,372,253.12 ikiwa ni sawa na 50.37% ya lengo la mwaka la kukusanya/kupokea jumla ya Tzs 53,232,913,555.00 kutoka vyanzo vyake mbalimbali vya ndani na Serikali kuu ikiwa ni pamoja na bakaa.

Mwenyekiti aliwahoji wajumbe kama wanapokea taarifa hiyo, Wajumbe waliipokea wakaijadili na kuhoji yafuatayo :-

i. Walihoji Suala la Afisa mapato aliyehama ambae alichukua fedha mbichi kwa Mtendaji wa kijiji cha Mulaga kata ya Buyagu Ndugu Matambo Jiji Kitwanga. Mkurugenzi mtendaji alieleza kuwa hakuwa na taarifa hiyo aliahidi kulifatilia ili kujua uhalisia wa suala hilo.
ii. Walihoji ni lini Uzio wa Mnada wa Sima utatengenezwa. Mkurugenzi Mtendaji alieleza kuwa Mnada wa Sima ni miongoni mwa vipaumbele vya Halmashuri vilivyo kwenye mpango wa matengenezo, tayari ujenzi umeanza upo hatua ya msingi na ujenzi utakamilika haraka iwezekanavyo kadri Fedha zitakavyopatikana.
iii. Walihoji suala la Mapato kushuka kuliganisha na makisio yaliyowekwa. Mkurugenzi alieleza kuwa mapato yanakusanywa ila kuna vyanzo vingine ambavyo msimu wake ulikuwa haujafika ikiwemo mazao ya kilimo. Aliongeza

kuwa Jitihada zinaendelea kufanyika ikiwa ni pamoja na kuajiri wakusanya mapato wapya 20 ili kuleta ufanisi kwenye ukusanyaji wa mapato. Mhe Mbunge wa Jimbo la Sengerema aliongeza kuwa Waheshimiwa Madiwani watanakiwa kujua POS zote zinazokusanya mapato na walio na POS hizo. Aidha aliwataka wataalam wafuatilie wajuwe CRS ya daraja la Busisi inalipwa wapi na ni kiasi gani Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema inadai kiasi gani kutoka kwenye mradi huo.

iv. Walihoji juu ya Ushuru wa Huduma ambao wafanyabiashara wanadaiwa miaka 3 nyuma.
    - Kama elimu ya kodi inatolewa kwa wafanyabiashara na kuwaelimisha wafanyabiashara kujua risti za Halmashauri
    - Walitaka kufahamu Ushuru wa Huduma inayopatikana kutokana na Mgodi wa Sotta Gold Mining.
    - Mkurugenzi Mtendaji alieleza kuwa mfumo unaonesha kwamba kuna baadhi ya Wafanyabiashara wanadaiwa miaka 3 hawajalipa Ushuru wa Huduma, suala la mafunzo kwa wafanyabiashara alieleza kuwa yanafanyika na yanaendelea kufanyika ili kuwaelimisha wajue umuhimu wa kulipa kodi ya Serikali pamoja na kujua Risiti za Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema, kuhusu Ushuru wa Huduma kutoka Mgodi wa Sotta Gold Mining, Mgodi bado haujaanza uzalishaji hivyo Makampuni yanayofanya kazi katika mgodi huo ndio yanalipa Ushuru wa Huduma.

v. Walihoji kuhusu malalo kwa sababu yaliyopo yamejaa. Mkurugenzi Mtendaji alieleza kuwa amelichukuwa kwa utekelezaji.

Baaada ya majadiliano hayo, Wajumbe walielekeza kuwa kuhusu eneo la malalo, Mkurugenzi Mtendaji pamoja na Wataalam wahakikishe eneo hilo linapatikana kwa sababu yaliyopo yamejaa. Vile vile Mkurugenzi Mtendaji pamoja na Wataalam wafatilie CRS kwenye daraja la Busisi ili ijulikane Halmashauri inadai kiasi gani cha fedha na ijulikane zinalipwa lini fedha hizo. Kisha wajumbe waliridhia taarifa hiyo.

***Azimio.2***
***Iliazimiwa kuwa Mkurugenzi Mtendaji (W) afuatilie suala la CRS ya daraja la Busisi inalipwa wapi na Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema inadai kiasi gani kutokana na mradi huo.***

***Azimio. 3***
***Iliazimiwa kuwa Mkurugenzi Mtendaji ahakikishe eneo jipya la malalo linapatikana kwa sababu maeneo yaliyopo yamejaa.***

TAARIFA YA MAGARI NA MTAMBO WA HALMASHAURI

Jumla ya Magari 10 yalifanya kazi mbali mbali ikiwemo kuwawezesha wataalam na Viongozi kutekeleza majukumu ya Serikali, Wajumbe walishauri kuwa Mtambo utengenezwe ili uanze kufanya kazi zilizokusudiwa. Waliongeza kuwa Mhe; Diwani wa kata ya Katunguru, mwenyekiti wa kijiji cha Nyamatongo na Afisa Usafirishaji (W) wafike Songolo marine kwa ajili ya kufanya tathimini ya utengenezaji wa boti ya juma kisiwani iliyopo kwenye gereji hiyo. Kisha waliridhia taarifa hiyo.

***Azimio: 4***
***Iliazimiwa kuwa Mhe; Diwani wa kata ya Katunguru, mwenyekiti wa kijiji cha Juma Kisiwani na Afisa Usafirishaji (W), wafike Songoro marine kwa ajili ya kufanya tathimini ya utengenezaji wa boti ya Juma Kisiwani iliyopo kwenye gereji.***

**Muht.Na.24/02/2024 - Kupokea Taarifa kutoka Taasisi mbalimbali.**
**Muht.Na.24/02/2024 (I) - Taarifa ya TANESCO.**
Kaimu Mkuu Meneja TANESCO aliwasilisha taarifa ya utendaji kazi wa Shirika la Umeme Tanzania, alieleza kuwa kazi ya kupeleka umeme katika vijiji vyote vya Halmashauri ya Sengerema imekamika kwa asilimia 100 na jumla ya vitongoji 213 vimepatiwa umeme, Jumla ya vitongoji 208 bado havijapatiwa umeme. Zoezi la kuhakikisha kila kitongoji kinapata umeme ndani ya miaka 5, ambapo tayari vitongoji 15 kati ya 208 vipendekezwa kwa ajili ya kupelekewa umeme. Aidha kuanzia Julai hadi Disemba 2023 jumla ya wateja 1,902 wameunganishiwa umeme ikiwa ni sawa na 109%. Vile vile kuna ofisi zinazotoa huduma za dharula kwa Wananchi viunga vipya (Clusters) katika maeneo ya Nyatukala, Kamanga, Busisi, Ngoma "A" na Kijiweni.
Wajumbe walipokea taarifa hiyo, wakaijadili waliwapongeza Shirika la Umeme kwa kazi nzuri wanayofanya ndani ya Halmashauri ya Sengerema. Wajumbe walihoji yafuatayo:- Eneo la Buyagu ya zamani umeme umeunganishwa lakini hauwaki, Mradi wa Umeme Magutu kwenye Trasfoma taa haziwaki, Eneo la Juma Kisiwani nguzo za umeme hazijafika na umeme hakuna, Kata ya Mwabaluhi eneo la Zanzibar haina umeme.
**Kaimu Mkuu Meneja TANESCO;** alieleza kuwa katika maeneo ya Buyagu ya zamani na Ibondo wananchi waliounganishwa ni wachache kwa ajili ya majaribio kama taratibu zinavyoelekeza, muda wa majaribio ukiisha kaya zote zitaunganishiwa umeme. Suala la taa ya Trasfoma kutokuwaka lilichukuliwa kwa ufatiaji zaidi. Aliongeza kuwa Suala la Juma kisiwani na Zanzibar wananchi waelimishwe ili wawe wavumilivu kusubiri Bajeti itakapotolewa, umeme utawaka maeneo hayo. Kisha waliridhia taarifa hiyo.

**Muht.Na.24/02/2024 (II) - Taarifa ya RUWASA.**
**Kaimu Mkuu Meneja RUWASA;** aliwasilisha taarifa ya utendaji kazi ya RUWASA, alieleza kuwa hali ya huduma ya Maji kwa Wilaya ya Sengerema ni 65% na miradi inayoendelea ikikamilika huduma ya Maji itafikia 85%. Mwenyekiti aliwahoji Wajumbe kama wanaipokea taarifa hiyo, Wajumbe waliipokea kisha akawakaribisha kwa majadiliano.
Wajumbe walihoji yafuatayo:-

i. Mradi wa maji kata ya Busisi ni mdogo ila unaudumia watu wengi kiasi kwamba unazidiwa uwezo, pia maji yanatoka yakiwa machafu yasiyofaa kwa matumizi.
ii. Mradi wa Maji Nyamililo uliyokuwa chini ya RUWASA umekabidhiwa kwa SEUWASA bila ya viongozi wa kijiiji husika kuhusishwa, hivyo makabidhiano hayo yafanyike tena na viongozi wa Kijiji pamoja na Madiwani wa Kata ya husika wapewe taarifa ili kushiriki makabidhiano hayo.
iii. Mradi wa Maji Kasungamile, Nyampande na Tabaruka maji hayatoki mara kwa mara, pia mradi wa maji wa Chamabanda - Kasungamile ndo unafikisha maji katika gereza za Kasungamile lakini mara nyingi Gereza la Kasungamile hawapati maji.

iv. Pampu ya maji iliyokuwa tunyenye iliamuliwa irudishwe kwenye kisima kilichopo Kishinda centre lakini bado haijarudishwa.
v. Kero ya Akaunti za maji kushindwa kufanya kazi kwa wakati hali inayopelekea Wananchi kukosa huduma ya maji kwa sababu ya kushindwa kununua umeme pamoja na kulipa posho.
vi. Kata ya Chifunfu kuna mitaro ambayo wananchi walichimba kwa ajili ya kuweka mabomba ya maji, muda mrefu umepita mabomba hayo hayajawekwa.

**Kaimu Mkuu Meneja RUWASA**; alieleza kuwa mradi wa maji Busisi kweli ni mdogo ila unasubiri bajeti ili kupanuliwa kwa Mradi huo, suala la maji machafu alilichukua kwa ufuatiliaji wa kina. Aidha aliahidi kuwa makabidhiano ya mradi wa maji wa Nyamililo kati ya RUWASA na SEUWASA yatafanyika tena mbele ya viongozi pamoja na Wahe, Madiwani. Mradi wa Maji Kasungamile, Nyampande na Tabaruka maji, Mhe: Mbunge Jimbo la Sengerema alieleza kuwa mradi huo utajengewa matenki yenye thamani ya takribani Milioni 730 ikiwa ni pamoja na mradi wa maji Kasomeko na Chamabanda ili kuwezesha miradi hiyo kufikisha maji kwa wananchi kwa ubora mkubwa. Kwa upande wa Pampu ya maji tayari imefika kwenye Kisima kilichopo Kishinda Centre.Suala la mfumo wa Akaunti ya Maji wahusika wawe wanafanya mchakato wa malipo mapema ili kuondoa usumbufu wa kuchelewa kwa malipo. Kuhusu kata ya Chifunfu fedha ikipatikana mabomba yatawekwa na kuanza kutoa huduma ya maji.
Hata hivyo Mhe: Mbunge Jimbo la Sengerema alishauri kuwa ni vyema kukawa na kikao cha pamoja cha Waheshimiwa Madiwani na Bodi za maji za SEUWASA na RUWASA pamoja na wakandarasi wa miradi ya Maji ili kujadili kwa pamoja kuhusu miradi ya maji. Kisha waliridhia taarifa hiyo.

**Muht.Na.24/02/2024 (III) - Taarifa ya SEUWASA.**
Taarifa hiyo haikuwasilishwa.

**Muht.Na.24/02/2024 (IV) - Taarifa ya TARURA.**
Meneja TARURA aliwasilisha taarifa ya utendaji kazi wa TARURA: Alieleza kuwa Halmashuuri ya Sengerema kwa mwaka wa fedha 2023/2024 imepangiwa jumla ya Tzs 2,513,240,000.00 kwa ajili ya matengenezo ya barabara, Mwenyekiti aliwahoji Wajumbe kama wanaipokea taarifa hiyo, Wajumbe waliipokea, wakaijadili. Wajumbe walihoji suala la matengenezo ya barabara zilizopo katika Kata ya Kishinda, Barabara hizo zimekatika kwa kuharibiwa na maji, vile vile wajumbe waliwasilisha maombi ya barabara katika kata zao. Mhe: Mbunge aliwaeleza Wajumbe kuwa wawe na subira Serikali inaleta fedha kwa ajili ya matengenezo ya barabara ikiwemo barabara ya kutoka Tabaruka hadi Kishinda na barabara ya Bukala- Ibondo. Kisha waliridhia taarifa hiyo.

**Muht.Na.25/02/2024:- Masula ya Nidhamu kwa Waheshimiwa Madiwani.**
**Katibu;** aliwasilisha agenda ya Masula ya Nidhamu kwa Waheshimiwa Madiwani, alieleza kuwa Tuhuma mbili zinazohusu Waheshimiwa Madiwani ziliwasilishwa katika Baraza la Nidhamu la waheshimiwa Madiwani. Hata hivyo Baraza la Waheshimiwa Madiwani lilijigeuza na kuwa Kamati. Baraza hilo lilihitimisha kwa kutoa maamuzi juu ya tuhuma zote Mbili. Kwa ufafanuzi Zaidi taarifa ya hitimisho la tuhuma hizo inapatikana katika faili la Siri "**Madiwani Complains**".

**Muht.Na.26/03/2024: - Kufunga kikao.**

**Katibu:** aliwashukuru wajumbe wote kwa ushirikiano, Alieleza kuwa Wataalam wanafanya kazi nzuri kutokana na ushirikiano mkubwa wanaopewa na Waheshimiwa Madiwani. Aliongeza kuwa shukrani za pekee ni kwa Mhe: Mbunge Jimbo la Sengerema, Mhe Tabasabu H. Mwagao kwa juhudi kubwa anazozifanya katika kuleta maendeleo wa wananchi wa Sengerema. aidha aliongeza kuwa changamoto zote zilizobainika kwenye Kata zitafanyiwa kazi vile vile maelekezo yote yaliyoelekezwa katika kikao yamechukuliwa kwa ajili ya utekelezaji. Kisha alimkaribisha Mwenyekiti kwa ajili ya itifaki za kufunga Kikao.

**Katibu wa UWT kwa niaba ya Katibu wa Chama cha Mapinduzi (W) ya Sengerema:**
Alianza kwa kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe: Dr. Samia Suluhu Hassan kwa kuleta fedha nyingi za miradi ya Maendeleo kwa Wananchi wa Wilaya ya Sengerema, ikiwa ni sambasamba na Mhe, Mbunge Jimbo la Sengerema, Mhe Tabasabu H. Mwagao kwa umoja wao wamefanya makubwa kwa Wananchi wa Sengerema. Alieleza kuwa Ilani ya chama cha mapinduzi inaelekeza kumtua mama ndoo kichwani hivyo wahusika watekeleze kwa vitendo ili kuwapunguzia wanawake adha ya kufata maji umbali mrefu.
**Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi (W) ya Sengerema:** aliwashukuru wajumbe kuendelea kutekeleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi. Hata hivyo alishauri kuwa Wahe: Madiwani waliomba Mkutano wa Baraza ufanyike siku mbili ili wapate muda wa kutosha kujadili taarifa za kwenye Kata zao. Aliongeza kuwa Wahe; Madiwani washiriki katika zoezi la uchaguzi mdogo katika kata ya Buzilasoga.

**Mkuu wa Wilaya ya Sengerema:** Aliwashukuru wajumbe, na kipekee alimshukuru Raisi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe: Dr. Samia Suluhu Hassan kwa maendeleo makubwa anayoyafanya kwa Watanzania wote, pamoja na miradi mikubwa ya maendeleo kwa Wananchi wa Wilaya ya Sengerema. Aidha aliwataka wasimamizi wa fedha za miradi kuhakikisha zinafanya kazi zilizokusudiwa. Aliongeza kuwa tarehe 14-15/03/2024 Mkuu wa Mkoa anategemea kufanya ziara kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema katika Kata ya Igalula hivyo wahusika wajipange kwa ajili ya ziara hiyo. Alisisitiza suala la usafi wa mazingira ili kuepukana na magonjwa yanayotokana na uchafu kama vile kipindupindu.

**Mwenyekiti:** Aliwapongeza ofisi ya Chama cha Mapinduzi (W), Ofisi ya Mhe: Mbunge Ofisi Mkuu wa Wilaya na Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W) kwa ushirikiano wao. Alisisitiza Menejimenti kuzingatia maelekezo ya yaliyotolewa na Mkutano wa Baraza la Waheshimiwa Madiwani, pia alisisitiza kuwa suala la ukusanyaji wa mapato litiiliwe maanani ili kufikia malengo na makisio yaliyowekwa. Kisha alifunga Mkutano saa 12:38 jioni.

.................................... ..............................

Makoye L. Sengelema
**MWENYEKITI**

Binuru M. Shekidele
**KATIBU**

**UMETHIBITISHWA LEO TAREHE**...10/05/2024.....